**MAFUNDISHO YA BIBLIA**

**kwa WATOTO wa**
**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**SikuYa Saba (7th day)**

---

**RoboYaTatu**
**2018**

---

**Ya**
**Aprili, Mei, Juni.**
**(TAMMUZ, AV, ELUL, TISHRI)**
**Kutumiwa na Biblia**

---

**Watendakazi wanahitajika, Mavuno ni mengi,**
**Lakini watenda kazi ni wachache...**

---

**Tuma maombi yote kwa,**
**3RD ANGEL MESSENGER**
**S.L.P. 9774**
**NAKURU.**
**3rdangelmessenger@gmail.com**

**SIMU: +254 721576325/+254 704590649**

---

**SOMO LA JULAI 7, 2018**

**AMRI KUMI**

*SomoKuu: Kumbukumbu La Torati 5:1-22*
*Fungu La Kukariri: Ufunuo14:12*

1. Ni nani alipeana Amri Kumi? Kutoka 20:1-4
2. Ni nani aliziandika? Kutoka 31:18
3. Je, Masihi alizitupilia mbali alipokuja ulimwenguni? Mathayo 5:17-18
4. Tukizishika amri hizi, je, tutakuwa na uzimawa milele? Mathayo 19:16-17
5. Je, tumeruhusiwa kutoshika baadhi ya hizo Amri kumi? Yakobo 2:10-11
6. Ni nani wataruhusiwa kuingia Mji ule Mtakatifu? Ufunuo 22:14(K.J.V)
7. Watakatifu ni nani? Ufunuo 14:12

**SOMO LA JULAI 14, 2018**

**KUJA MARA YA PILI KWA MASIHI**

*SomoKuu: MatendoYaMitume1:1-12*
*FunguLa Kukariri: MatendoYaMitume1:11*

1. Masihi atarejea mara ya pili? Waebrania 9:28
2. Je, Masihi aliahidi kuja tena mara ya pili? MatendoyaMitume 1:11
3. Alimjibu vipi mmoja wa mitume wake kuhusukujakwakemaraya pili? Yohana 14:1-3
4. Akija mara ya pili, je tutawala naye? Ufunuo 20:4
5. Nabii ZEKARIA alitabiri vipi kuhusu kurudi mara ya pili kwa Masihi? Zekaria 14:1-9
6. Je, watu wote waliohai watamuona? Ufunuo 1:7
7. Ninikitafanyika kwa wale waliokufa wakiwa ndani yake? Na pia wale watakaokuwa hai ndani yake atapokuja? 1 Wathesalonike 4:16-17

**SOMO LA JULAI 21, 2018**

**MAMBO AMBAYO HATURUHUSIWI KUYAFANYA KATIKA SABATO**

*SomoKuu: KumbukumbuLa Torati5:1-20*
*FunguLa Kukariri: Isaya58:13*

1. Usifanye kazi ya Kawaida siku ya Sabato. Isaya 58:13; Amosi 8:5-7; Nehemia 13:15-22
2. Usifanye mambo yaanasa...Isaya 58:13
3. Usione Sabato kuwa niutumwa… Amosi 8:5-7
4. Usikose kwenda Kanisani… Walawi 23:3; Luka 4:16;
5. Usikose kumsaidia mtu mwenye njaa au mgonjwa… Yakobo 2:14-17; Mathayo 12:11-12

6. Usiogope kutumia kipawa chako… 1 Wakorinitho 12:4-7; 1 Timotheo 4:14
7. Usifanye biashara siku ya Sabato… Nehemia 13:15-22; 10:31

**SOMO LA JULAI 28, 2018**

**NYAMA SAFI NA NYAMA ISIYO SAFI**

*SomoKuu: Walawi11:1-23*
*FunguLa Kukariri: Walawi20:25*

1. Je, tumekubaliwa kula kila Nyama? Walawi 20:25
2. Isopokuwa katika kitabu cha Walawi, nimahali pengine wapi tunapata jambo hili? Kumbukumbu la torati 14:3-20
3. Nabii Isaya amesema vipi kuhusu watu wanaokula nyama najisi kama Nguruwe naPanya? Isaya 66:17
4. Katika agano jipya jambo hili limenenwa vipi? 1 Tomotheo 4:4-5
5. Nuhu aliamriwa aje kuhusu jambo hili? Mwanzo 6:21
6. Nuhu alifuata amri hii? Mwanzo 8:20
7. Je, twafaa kufuata jambo hili? Warumi 15:4

**SOMO LA AGOSTI 4, 2018**

**KUTII**

*SomoKuu: I Samueli15:1-35*
*FunguLa Kukariri:1 Samueli15:22*

1. Elohim amenena aje kuhusu uasi (kutotii)? 1 Samueli 15:23
2. Tukitaka kumpendeza Elohim twafaa kufanya nini? 1 Samueli 15:22
3. Je, Manabii walimtii Elohim? 1 Samueli 3:10; Hosea 4:2-3
4. Je, Masihi alipata kupendwa na watu pamoja na Elohim kwa kutii kwake? Luka 2:52
5. Je, watu watakatifu wameamriwa kutii Elohim kwakuzishikaAmri kumi? Ufunuo 14:12
6. Ni kwa njia ipi twaonyesha upendo wetu kwa Elohim? Yohana 14:15
7. Je, watoto wameamriwa kutii wazazi wao? Waefeso 6:1

**SOMO LA AGOSTI 11, 2018**

**MITUME WA MASAHI**

*SomoKuu: Mathayo10:1-16*
*FunguLa Kukariri: Mathayo10:2-4*

1. Majina ya mitume wa Masihi ni yapi? Mathayo 10:2-4

2. Wakati Masihi alipowatuma, aliwaambia vipi kuhusu ufalme wa mbinguni? Mathayo 10:7
3. Ni nguvu ipi walipewa? Mathayo 10:8
4. Kwa hao mitume wake niyupi alimsaliti? Mathayo 10:4
5. Nani alirudi mahali pa yule aliyemsaliti? MatendoyaMitume 1:26
6. Baada ya Masihi kupaa mbinguni, je mitume wake waliendelea kuponya wagonjwa? Matendo ya Mitume 5:15
7. Kama wafuasi wa Masihi je tutapewa nguvu za uponyaji kam awalivyopewa? Mariko 16:17-18

**SOMO LA AGOSTI 18, 2018**

**JE, MTU MTAKATIFU AKIFA, HUENDA MBINGUNI?**

*SomoKuu: Webrania11:1-40*
*FunguLa Kukariri: Waebrania11:39*

1. Je Habili alihesabiwa kuwa mwenye haki baada ya kutoa Sadaka? Waebrania 11:4
2. Je, alipokufa, aliendaMbinguni? Mwanzo 4:9-10
3. Paulo anasema vipi kuhusu wenye haki, watafufuka au wameshafufukatayari? MatendoyaMitume 24:15
4. Masihi alisema vipi kuhusu wale waliokufa wakiwa watakatifu? Yohana 5:28-29
5. Katika Kitabu cha Danieli, watakatifu wako wapi? Danieli 12:2
6. Waliokufa katika Masihi parapanda itakapolia watatokea wapi? 1 wathesalonike 4:16
7. Wakati Paulo alimaliza maisha yake, je aliahidiwa kuenda mbinguni? 2 Timotheo 4:7-8

**SOMO LA AGOSTI 25, 2018**

**JE, MTU MWENYE DHAMBI AKIFA, HUENDA KWENYE ZIWA LA MOTO?**

*SomoKuu: Ufunuo20*
*FunguLa Kukariri: MatendoYaMitume24:15*

1. Waliokufa wakiwa wenye dhambi wako wapi? Ufunuo 20:4-5
2. Tunaona wakitoka wapi ili wahukumiwe? Ufunuo 20:13-15
3. Je, mwenye dhambi aweza kutubu baada ya kufa? Zaburi 6:5
4. Mhubiri ananena vipi kuhusu jambo hili? Mhubiri 9:10
5. Ayubu anesema watu huenda wapi wakifa? Ayubu 14:10-12
6. Huwa tunasoma vipi katikaWaebrania 6:2? Waebrania 6:2
7. Mtu alikuwa aende wapi akifa? Mwanzo 3:19

## SOMO LA SEPTEMBA 1,2018

## UNABII WA BIBLIA

*SomoKuu: 2 Petero1:19-21*
*FunguLa Kukariri: Amosi3:7*

1. Je, tunaweza kutafsir iunabii katika bibilia tukitumia hekima yetu? 2 Petero 1:20
2. Katika unabii Maji yanasimamia nini? Ufunuo 17:15
3. Mnyama au Wanyama inasimamia nini? Danieli 7:17
4. Mwanamke anasimamia nini? Waefeso 5:23-32
5. Upepo unasimamia nini? Yeremia 23:19
6. Ufunuo ulipewa nani? Ufunuo 1:1
7. Je, kuna baraka ya kusoma, kusikiza na kutunza maneno ya unabii? Ufunuo 1:3

## SOMO LA SEPTEMBA 8,2018

## UBATIZO

*SomoKuu: Yohana 3:1-12*
*FunguLa Kukariri: Yohana 3:3*

1. Masihi alisema vipi kuhusu ubatizo? Yohana 3:3
2. Mitume wa Masihi walibatiza vipi? MatendoyaMitume 2:38; 19:5
3. Je, Masihi alibatiza watoto? Mathayo 19:13-15
4. Wakati Masihi alikuwa mtoto, je alibatizwa? Luka 2:25-29
5. Mtu hubatizwa vipi? Matendo ya Mitume 8:38; Mathayo 3:16; Warumi 6:3-4
6. Ni aina ngapi za ubatizo zimeelezwa katika Maandiko? Waefeso 4:5
7. Baada ya ubatizo je, tumeruhusiwa kufanya dhambi na kubatizwa tena? Waebrania 10:26-29

## SOMO LA SEPTEMBA 15, 2018

## KUISHI KAMA MASIHI

*SomoKuu: Luka 2:40-52*
*FunguLa Kukariri: Wafilipi2:5*

1. Je, mitume waMasihi walimuiga? 1 Wakorinitho 11:1
2. Je, Masihi alizishika amri? Yohana 15:10
3. Ombi la Masihi kwa wafuasi wake lilikuwa lipi? Yohana 17:9
4. Maisha yake yalikuwa vipi? Alipokuwa mtoto mdogo? Luka 2:52
5. Ni ombi lipi aliwafunza wafuasi wake? Mathayo 6:9-14

6. Je, wafuasi wake watapata faida nyingi wakiishi ndani yake? Yohana 15:5
7. Nini anaahidi kwa wale watakaoishi kama alivyoishi? Ufunuo 3:21

## SOMO LA SEPTEMBA 22,2018

## AMRI YA TANO

*SomoKuu: Kutoka20:1-17*
*FunguLa Kukariri: Kutoka20:12*

1. Ni amri ipi iliyo na ahadi? Waefeso 6:1-2
2. Ahadi ni ipi? Waefeso 6:3
3. Twafaa kuwafanyia vipi watu wenye umri sawa au zaidi na baba zetu wazazi? 1 Timotheo 5:1(Sehemu ya Kwanza)
4. Tunafaa kuwafanyia vipi watu wenye umri sawa na mama zetu au zaidi? 1 Timotheo 5:2 (Sehemuya kwanza)
5. Tukiwatii wazazi wetu, je inaonyesha tunampenda Elohim? Yohana 14:15
6. Je, Masihi alitii hii amr ialipokuwa mtoto mdogo? Luka 2:51
7. Ni vigumu kutunza amri? 1 Yohana 5:3

## SOMO LA SEPTEMBA 29,2018

## PAULO YULE MTUME

*SomoKuu: MatendoYaMitume9*
*FunguLa Kukariri: MatendoYaMitume9:22*

1. Kabla ya kubadilika, Paulo alikuwa akifanya nini? Matendo ya Mitume 9:1-2
2. Nini kilifanyika kwake alipokuwa akisafiri kuenda Damesiki? Mtendo ya Mitume 9:3-4
3. Ni maneno yapi aliyasikia alipoanguka chini? Matendo ya Mitume 9:4
4. Ni Nani alikuwa ananena maneno hayo? Matendo ya Mitume 9:5
5. Ni Nani alitumwa kumuombea iliapate kuona tena? Matendo ya Mitume 9:10-12
6. Jina lake lilikuwa lipi kabla ya kubadilika? Mtendo ya Mitume 9:11
7. Ni kazi ipi alifanya ya kueneza injili? 1 Timotheo 2:7